



TANZANIA BASKETBALL FEDERATION (TBF)



FIBA
AFRICA
We Are Basketball

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

YAH: UCHAGUZI WA VIONGOZI

TAREHE: 01/01/2018

Shirikisho la Mpira wa kikapu nchini (TBF) limefanikiwa kupata safu mpya ya uongozi katika uchaguzi uliofanyika siku ya jumamosi tarehe 30/12/2017 katika ukumbi wa NAM Hotel mjini Dodoma. Uchaguzi ambao ulisimamiwa na Baraza la Michezo la Taifa (BMT) ambapo jumla ya mikoa 13 wanachama na jumla ya wajumbe 29 walipiga kura kuchagua viongozi wapya.

Jumla ya nafasi 9 za uongozi ziligombaniwa (i.e. Raisi, Makamu Raisi, Katibu Mkuu, Mweka Hazina na makamishna wa Mipango na Maendeleo, Ufundi na Mashindano, Walemavu, Watoto na Mashule, Waamuzi).

Kamati ya utendaji kwa kushirikiana na Bodi ilifanya mabadiliko ambayo yaliridhiwa na wajumbe wa mkutano mkuu katika nafasi za Katibu Mkuu Msaidizi na Kamishna wa Ufundi na Mashindano.

UONGOZI MPYA

1. RAISI - PHARES MAGESA
2. MAKAMU RAISI - MBOKA MWAMBUSI
3. KATIBU MKUU - MICHAEL MWITA
4. KATIBU MKUU MSAIDIZI - MANASE ZABLON
5. MWEKA HAZINA - AMINA AHMED
6. KAMISHNA MIPANGO - MICHAEL KADEBE
7. KAMISHNA WATOTO NA MASHULE - ABDALLAH MPOGOLE
8. KAMISHNA UFUNDI NA MASHINDANO - MWENZE KABINDA
9. KAMISHNA WALEMAVU - AZIZY MWARUKA
10. KAMISHNA WAAMUZI - ALFRED NG'HALALIJI

Shirikisho linapenda kutoa shukurani za dhati kwa mchango wa wadau wote walioshiriki katika kipindi chote cha uchaguzi katika kutangaza, kuhamasisha na kuelimisha jamii.

Pia linawaomba wadau wote kutoa ushirikiano katika kuhakikisha mchezo wa mpira wa kikapu unarejesha heshima yake kitaifa na kimataifa.

TANZANIA BASKETBALL FEDERATION
P.O. Box 42089
DAR-ES-SALAAM
TANZANIA

Michael Mwita
Katibu Mkuu (TBF)